



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO



23/10/2024

TANGAZO LA MKOPO KWA WATUMISHI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO KUTOKA HAZINA

Somo tajwa hapo juu lahusika.

Watumishi wote mnatangaziwa kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imepokea fedha kiasi cha **Tsh. Milioni mia nne (400,000,000/=)** kutoka Wizara ya Fedha (Hazina) kwa ajili ya kukopesha Watumishi. Mkopo huu hauna riba ukiwa na lengo la kuwawezesha Watumishi kupata vyombo vya usafiri na kutengeneza magari yao binafsi ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

TARATIBU ZA UTOLEWAJI WA MIKOPO

Mtumishi mwenye uhitaji na Mkopo huo atatakiwa kujisajili kwenye Mfumo wa Hazina Portal kupitia kiunganishi cha (als.muse.go.tz), kwa kutumia taarifa zake kama zilivyo kwenye taarifa zake za Kiutumishi kwenye mfumo wa **e-watumishi** na **ess**, kwa kufuata hatua zifuatazo:-

1. Baada ya kufungua kiunganishi cha als.muse.go.tz atabonyeza sehemu iliyoandikwa **kujiunga/register** kisha ataweka taarifa zake na kubonyeza sehemu imeandikwa **verify details**. Taarifa zikiwa sahihi utafunguka ukurasa wa pili kisha atabonyeza **continue with registration** kisha atakamilisha kwa kuweka taarifa za jumla (**general details**) zitakazomwezesha kutumiwa **link/kiunganishi** kwenye **email ambayo akiifungua/bonyeza ku-verify** itamtumia **namba/code** maalum kwa namba yake ya simu ili kukamilisha usajili na kuweza kuingia na kutuma maombi ya mkopo kwa mfumo wa **Hazina portal**.

2. Mtumishi aliyekamilisha usajili ataingia kwenye Mfumo kwa kuweka **cheke namba** na **neni la siri** alilotengeneza kikamilifu kisha ataenda kwenye kitufe cha **ADVANCE LOAN** na kisha kuomba mkopo.
3. Ili kukamilisha maombi na kutuma utatakiwa kubonyeza sehemu imeandikwa **Actions** kisha **more details** halafu **Submit**. Hapo mkopo utakuwa umekwenda kwa **Loan Representative/Mwakilishi wa mikopo** kwa hatua zaidi.


MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

Utoaji mikopo utazingatia mambo yafuatayo:-

- i) Lazima Mkopaji abakiwe na 1/3 ya Mshahara wake baada ya makato yote.
- ii) Mtumishi mwenye shauri la nidhamu haruhusiwi kuomba.
- iii) Mkopaji atalipia 3% ya service charge na 1% ya Bima ya Mkopo ambayo itakatwa mara moja tu wakati anapewa mkopo.
- iv) Mtumishi mwenye mkopo wa Hazina hataruhusiwa kukopeshwa mkopo mwingine kabla ya kukamilisha kurejesha mkopo wa awali.
- v) Fedha za mkopo zinalipwa kupitia akaunti ya Mshahara ya Mtumishi husika
- vi) Katika kushughulikia maombi ya waombaji wenye sifa, mfumo wa Hazina Portal unatumia utaratibu wa muombaji aliyewahi kuomba mwanzo ndio atahudumiwa kwanza (**FIFO - First In, First Out**) mpaka pale kiwango cha pesa kilichotengwa kitakapoishia.

Muhimu

Mwisho wa kupokea maombi ya mkopo ni tarehe 29 Oktoba, 2024 saa 05:59 usiku.


Prudence Kaaya-Ching'ole

Kny: Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri

nakala: Mkurugenzi Mtendaji - aione kwenye jalada

**Sub-DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
CHAMWINO DISTRICT COUNCIL
P. O. Box 1126
DODOMA**